**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

S.L.P 1951, Moshi-Kilimanjaro

Simu: 027-2750885; Nukushi:027- 2750889

Barua pepe: rbckilimanjaro@pccb.go.tz

Wavuti: www.pccb.go.tz

---

**KILIMANJARO – JULAI 22, 2020**

# TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KIPINDI CHA APRILI –JUNI 2020 KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

## VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA WAASWA KUTOKUJIHUSISHA NA RUSHWA KUELEKEA UCHAGUZI MKUU 2020.

TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro imeshiriki katika semina za siasa na Halmashauri Kuu za CCM Wilaya na Mkoa kwa kutoa mada ya mapambano dhidi ya Rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais wa Oktoba 2020 na kuwaasa viongozi wa Chama na wajumbe wa CCM ambao ndio wapiga kura kuchagua wawakilishi wa Chama katika kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu ujao wa 2020 kutojihusika kabisa na vitendo vya rushwa.

Kujihusisha na vitendo vya rushwa kunaleta makundi, mgawanyiko katika chama na uteuzi wa wawakilishi dhaifu na wasio na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha. Ushiriki katika semina hizi ni utekelezaji wa jukumu la TAKUKURU la Kuzuia Rushwa nchini. "TAKUKURU haitasita kutekeleza jukumu lake la pili la kupambana na Rushwa kwa wale ambao hawatataka kusikiliza yale wanayokatazwa" alisisitiza Mkuu wa TAKUKURU (M) wa Kilimanjaro, Bw. Fidelis Kalungura.

**TAARIFA ZILIZOPOKELEWA:**

Katika kipindi hiki cha miezi mitatu (Aprili – Juni, 2020) tulipokea taarifa 196, kati ya hizo zilizoonekana kuwa za makosa ya rushwa ni **117** na ambazo hazina uhusiano na makosa ya rushwa ni **79** ambazo zilihamishiwa katika idara nyingine.

**Mchanganuo wa taarifa**

1. Tamisemi – 96

- *Serikali za mitaa 45*
- *Halmashauri 30*
- *Afya 14*
- *Elimu 07*

2. Ushirika 15
3. Ardhi 15

4. Vyama vya siasa 12
5. Polisi 09
6. Mahakama 07
7. Hifadhi za jamii 07
8. Ujenzi 03
9. Maji 03
10. Bima 01
11. TRA 01
12. Uhamiaji 01
13. Sekta binafsi 23

Taarifa zote za makosa ya Rushwa zimefanyiwa kazi na uchunguzi upo katika hatua mbalimbali za kiutawala.

**MASHTAKA**

Mashauri mapya yaliyofikishwa mahakamani ni **kumi na moja (11)** ambayo ni kama yafuatavyo:-

1. **CC.239/2020** inayomhusu **Anneth Charles Kimaro** ambaye ni karani wa Tumaini SACCOS ya mjini Moshi anayetuhumiwa kwa kughushi na kuiba Tshs 3,650,000/=. Kesi hii ipo Mahakama ya Wilaya ya Moshi na ilifunguliwa mnamo 8.6.2020,

2. **CC.51/2020** inayomhusu **Aston Elinazi Mgonja** ambaye ni Diwani Kata ya Mpiji wilayani Same akituhumiwa kwa kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu kiasi cha Tshs 3,000,000/ kutoka kwa wananchi wa kijiji cha Gundushi. Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Same na ilifunguliwa mnamo 29.4.2020,

3. **CC.141/2020** inayomhusu **Benedict Kimaro** ambaye ni mshauri wa mahakama akituhumiwa kwa kuomba na kupokea hongo ya shs 100,000/= ili ashauri kutoa upendeleo kwenye shauri 121/2020 Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi na ilifunguliwa mnamo 17.04.2020,

4. **CC.203/2020** inayomhusu **Richard Meela** ambaye ni mfanyabiashara mjini Moshi akituhumiwa kwa kughushi taarifa ya fedha ya benki ya Stanbic na kujaribu kujipatia kiasi cha tshs 156,000,000/ Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi na ilifunguliwa mnamo 14.05.2020.

5. **CC.68/2020** inayomhusu **Godlisten Kundael Munisi** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Kirua katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha akituhumiwa kwa kuomba na kupokea hongo ya shs 20,000/= ili asichukue hatua kwa kosa la kukata miti bila kibali Kesi hii ipo

katika Mahakama ya Wilaya ya Siha na ilifunguliwa mnamo 11.06.2020,

6. **CC.02/2020** inayomhusu **Christon Elia Nkya na mwenzake** ambao ni Afisa afya na Mfamasia katika Halmashauri ya wilaya ya Rombo wakituhumiwa kwa kughushi hati ya mauzo no 10023 kutoka kitengo cha madawa (msd) na kujipatia kiasi cha 1,558,000/= Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Rombo na ilifunguliwa mnamo 02.06.2020,

7. **CC.97/2020** inayomhusu William Richard Mmbaga ambaye ni mfanyabiashara wilayani Mwanga akituhumiwa kwa kutoa hongo ya shs 25,000/= kwa mtoa taarifa ili aweze kuondoa tuhuma za kutotii sheria katika shauri la RB/112/2020 liliripotiwa kituo cha polisi Mwanga . Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Mwanga na ilifunguliwa mnamo 16.06.2020.

8. **ECC.04/2020** inayomhusu **Hassan Mkwizu na wenzake** ambaye ni Afisa Utumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga akituhumiwa kwa kughushi na kujipatia fedha kiasi cha Tshs 9,500,000/ katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 . Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Mwanga na ilifunguliwa mnamo 04.06.2020.

9. **CC.96/2020** inayomhusu GERALD ELIEKA LYIMO ambaye ni mhasibu msaidizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai akituhumiwa kwa kughushi na kujipatia fedha kiasi cha Tshs 5,125,000. Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Hai na ilifunguliwa mnamo 15.05.2020.

10. **CC.65//2020** inayomhusu IPYANA MWAIPOPO NGOJO ambaye alikuwa mhasibu wa H/W Siha akituhumiwa kwa wizi wa kiasi cha Tshs 2,030,000/ mali ya H/W Siha .Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Siha na ilifunguliwa mnamo 5.06.2020.

11. **CC 50/2020** inayomhusu EMILY GREYSON MHINA ambaye alikuwa ni fundi umeme akituhumiwa kwa kujipatia fedha kwa njia za wizi kiasi cha Tshs 2,065,000/ kutoka kwa wananchi wa kijiji cha Gundusine ili aweze kuwasaidia kuunganishiwa umeme. Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya SAME na ilifunguliwa mnamo 28/.04.2020.

Mashauri yaliyokamilika ni matano (05) ambapo tulishinda matatu **(03)** na kushindwa mawili **(02)**

**Mashauri tuliyoshinda ni;**

**1. CC 02/2018; JAMHURI DHIDI YA JAMES MERISHO**

Huyu alikuwa ni Afisa Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na alituhumiwa kwa kuomba na kupokea hongo ya shs 100,000/= ili, alihukumiwa kwa kosa la hilo kuomba na kupokea hongo shs 100,000/= kwenda jela miaka miwili (2) au kulipa faini ya shilingi laki tano (500,000/=) kwa kila kosa. Alilipa shilingi laki tano (500,000/=) na kuwa huru,

**2. CC540/2017; JAMHURI DHIDI YA NICODEMUS LEO NYAKI**

Huyu alikuwa ni Afisa Manunuzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ambaye alishtakiwa kwa makosa chini ya vifungu vya 333, 335 na 337 vya sheria ya kanuni za adhabu na kifungu 22 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa ubadhirifu wa shs 5,120,000/= na alitiwa hatiani na kutakiwa kwenda jela miaka miwili (02) au kulipa faini shilingi milioni moja (1,000,000/=), alilipa faini na kuachiwa huru.

**3. CC 03/2019; JAMHURI DHIDI YA SAFIEL ELIAS MJEMA**

Huyu alikuwa ni Mwamuzi wa mpira wa miguu daraja la pili wa mjini Moshi ambaye alishtakiwa kwa kosa la kuomba na kupokea hongo kiasi cha shilingi laki moja na alfu ishirini (120,000/=) ili aweze kutoa upendeleo kwa timu ya "New Generation" iliyokuwa ikicheza na timu ya La Familia kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa na. 11/2007 na alitiwa hatiani na kutakiwa kutumikia kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya shilingi laki tano (500,000/=). Mtuhumiwa alishindwa kulipa faini hiyo na hivyo alipelekwa jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja jela.

**FEDHA ZILIZOOKOLEWA**

Jumla ya **shs. 4,867,500/= (milioni nne, laki nane sitini na saba elfu na mia tano)** ziliokolewa katika kipindi cha Aprili – Juni, 2020 kama ifuatavyo;

- **Shs 997,500/=** zilirejeshwa kwenye akaunti ya Serikali na Mwenyekiti wa kamati ya pembejeo na wenzake,toka kijiji cha Kituri,wilaya ya Mwanga , fedha ya pembejeo waliyoifanyia ubadhirifu.
- **120,000/=** zilirudishwa na madiwani kwa kulipwa posho za

vikao bila kuhudhuria vikao na zimerudishwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

- **Shs 1,600,000/=** zilirejeshwa na mfanyabiashara wa eneo la Boma ng'ombe zikiwa ni fedha alizokuwa amejipatia pasipo kustahili kutokana na kukodisha eneo la TANESCO wilaya ya Hai.
- **Shs 1,550,000/=** zilirejeshwa kwa mwananchi na kampuni Mabena Microfinance ya Hai kumtoza riba ya kiwango cha juu (ijulikanayo kama mikopo umiza) kinyume cha sheria.
- **Shs 600,000/=** asilimia kumi ya mauzo ya ardhi kijiji cha Mongushi Hai iliyofanyiwa ubadhirifu na mwenyekiti wa kijiji na wenzake wawili kwa kutoiwakilisha katika serikali ya kijiji**.** Utaratibu za kurejesha fedha hizo serikali ya kijiji unaendelea .
- **Shs 1,000,000/=** zimerejeshwa kwa watumishi wa afya waliopunjwa stahili zao baada ya Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha ambaye ni Mhasibu Msaidizi kufanya ubadhirifu wa fedha hizo ambazo zilikuwa zimetolewa na shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama EGPAF.

## UZUIAJI RUSHWA

TAKUKURU imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali katika lengo kuu la kudhibiti rushwa nchini kwa kuhakikisha mifumo

mbalimbali ya utendaji kazi katika Taasisi za serikali inaimarishwa, taratibu, kanuni na sheria zinafuatwa na huduma bora za serikali zinatolewa. Mojawapo ya kazi zilizofanyika ni;

**Uchambuzi wa Mifumo**

i. Uchambuzi wa mfumo wa upangaji wa vibanda vya biashara vilivyoko katika kituo cha mabasi Moshi vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Baada ya kufanya uchambuzi huu imebainika kuwa ulifuata taratibu , kanuni na sheria za Manunuzi ya umma, malalamiko ya wazabuni yaliyoibuka kutokana na zabuni yalijibiwa kwa mujibu wa sheria na wazabuni ambao hawakuridhika na majibu hayo walifungua kesi Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Moshi na inaendelea hadi sasa hivi.

ii. Uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa hifadhi ya Msitu wa Rau uliopo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Baada ya uchambuzi baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni wanakijiji wanaoishi pembezoni mwa misitu kufanya uharibifu wa mazao ya misitu, biashara haramu kufanyika msituni ikiwemo biashara ya pombe haramu ya gongo, upitishaji wa mkaa, mafuta ya taa na mirungi katika njia inayopita katikati ya msitu , utaratibu ambao si mzuri wa ukusanyaji viingilio kwa wale wanaoingia msituni kwa ajili ya utalii na walinzi wa msitu wasio waadilifu. Ofisi imeazimia kufanya kikao na wadau wa msitu husika ikiwemo Wakala wa

huduma za Misitu Moshi (TFS), Afisa maliasili Mkoa, na kamati mbalimbali za utunzaji wa mazingira za kata na vijiji ili kuweza kuweka mikakati ya kuondoa changamoto zinazoukabili msitu.

**Ufuatiliaji wa Rasilimali za Umma**

i. Ufuatatiliaji wa mradi wa ujenzi wa daraja mto Kyarongo na barabara ya Kifura–Orera ulioko Mweka uliosimamiwa na TARURA Wilaya ya Moshi uliogharimu kiasi cha **Tshs 217,360,250/=** na kubaini kuwa eneo pembezoni mwa daraja limepata mmomonyoko wa udongo kutokana kuondolewa kwa uoto uliokuwepo wakati wa ujenzi hali inayohatarisha usalama wa daraja. Baada ya kufanya ufuatiliaji huu TARURA waliongeza nguvu katika eneo lililomomonyoka kwa kujenga tabaka mbili za mawe na saruji katika eneo husika

ii. Ufuatiliaji wa mradi wa uboreshaji wa hifadhi ya msitu wa Rau uliopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi uliogharimu kiasi cha USD 25,876 sawa na Tshs 52,062,700/= kwa kipindi hicho. Kiasi hiki kilifadhiliwa na UNDP kwa ajili ya kuboresha msitu tajwa na kilitumika kufanya ujenzi wa geti la kuingilia Msituni pamoja na kibanda/ofisi ya mlinzi pamoja na choo na pia kununua vifaa vya usalama kwa walinzi ikiwemo buti na sare zao, pia kukuza miche ya miti mbalimbali katika vitalu na kuipanda

msituni na kuutangaza misitu kupitia waandishi mbalimbali wa habari katika vyombo vya habari vilivyoko Moshi na Wilaya ya Hai.

iii. Ufuatiliaji wa mradi wa mradi wa umeme katika eneo la ORERA, MWEKA ambao ofisi ilipata malalamiko kuwa baadhi ya nyumba zilizokuwa kwenye ramani ya mradi husika hazijawekewa nguzo badala yake zimewekewa nyumba nyingine ambazo hazipo kwenye ramani. Baada ya kufuatilia kuhusu mradi husika ambao ulikuwa umetengewa Tshs 12,000,000/= na kupitia ramani ya mradi huo TANESCO Moshi na pia kutembelea mradi huo katika kitongoji cha ORERA, MWEKA ilibainika kuwa maeneo yote yaliyowekewa nguzo kwa ajili ya kuvutiwa umeme yako kwenye ramani na kuwa kuna maeneo yaliyoko kwenye ramani lakini hayawekewa nguzo kutokana na changamoto ya bajeti iliyotengwa kuwa ndogo na wananchi walioko katika maeneo hayo ndio wanaolalamika kuwa hawajafikiwa na huduma hiyo. TANESCO wanaazimia kukamilisha mradi huo katika bajeti ya 2020/2021 hivyo wananchi walishauriwa wavute subira.

## ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi hicho cha Aprili – Juni 2020, tumefanya semina ishirini (20) kwa makundi mbalimbali, mikutano ya hadhara hamsini na sita (56), uimarishaji wa Klabu za wapinga rushwa arobaini na tatu (43),

tumeendesha vipindi vya radio vitatu (03), tumeshiriki katika onesho moja (01) na tulitayarisha makala kumi na moja (11) kwa ajili ya machapisho yanayoandaliwa na TAKUKURU.

Elimu hii imeongeza uungwaji mkono kutoka kwa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa na hivyo kuwepo kwa taarifa nyingi za rushwa zilizopokelewa kama ilivyoelezwa hapo juu.

**MWELEKEO WA KIPINDI CHA KUANZIA JULY 2020.**

Nguvu zitaelekezwa katika ufuatiliaji rushwa katika uchaguzi ndani na nje ya vyama vya siasa ikiwa ni pamoja na uelimishaji wa mapambano dhidi ya rushwa katika kuelekea uchaguzi mkuu ujao wa madiwani, wabunge na Rais. Na pia tutaendelea kufuatilia fedha za miradi mbalimbali ambayo inagharamiwa na Serikali na wadau mbalimbali wanayofadhili miradi kwa jamii. Tunawaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU.

**Imetolewa na:**

**FEDELIS KALUNGURA**

Mkuu wa TAKUKURU (M) Kilimanjaro